TANGAZO LA SERIKALI Na. 164 la tarehe 13/6/2014

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA YA 288)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)

SHERIA NDOGO ZA (UDHIBITI WA UFUGAJI HOLELA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA DODOMA, 2014

Jina na mwanzo wa kutumika

1 Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Udhibiti wa Ufugaji Holela) za Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma za Mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa itakapoelezwa vmginevyo:-

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma.

"kijiji" maana yake ni Kijiji kilichoandikishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287.

"mazao" maana yake ni mazao ya aina yote yanayolimwa ndani ya eneo la Halmashauri;

"mifugo" maana yake ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe; farasi, punda pamoja na mnyama mwingine yeyote anayefugwa;

"mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri aliyetuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"msafara" maana yake ni njia iliyotengenezwa mahususi kwa ajili ya kupitisha mifugo;

"waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

Wajibu wa Halmashauri

4.-(1) Ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na udhibiti wa Mifugo inayozurura hivyo mjini Halmashauri itaandaa, kusimamia na kuhamasisha:-

(a) mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kuzingatia shughuli za Kilimo, Ufugaji na Makazi;

(b) inalinda mipaka ya ardhi ya makazi, kilimo na ufugiaji kama ilivyobainishwa katika mpango wa matumizi bora ya ardhi;

(c) kutoa vibali vya idadi ya mifugo ambayo mfugaji ataruhusiwa kufuga;

(d) wafugaji kuanzisha mpango wa "zero grazing";

(e) wafugaji kuvuna mifugo yao ili kubakisha idadi ya mifugo yenye kuleta tija;

(f) utoaji wa elimu ya ufugaji wa kisasa ili kuwa ufugaji wenye tija.

Wajibu wa Mfugaji

5.—(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mfugaji:-

(a) kuheshimu mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kufuata mipaka ya ardhi ya Kilimo, Ufugaji, Hifadhi za Barabara na shughuli nyingine;

(b) kufuga mifugo kulingana idadi na aina itakayoelekezwa na Halmashauri kwa kuzingatia ukubwa wa eneo lake la malisho;

(c) kuogesha na kuchanja mifugo yake kila mala na ili kuzuia magonjwa ya mifugo na magonjwa ya mlipuko;

(d) kupitisha mifugo yake kwenye njia maalum zilizotengwa kwa ajili ya mapitio ya mifugo wakati wa kwenda au kurudi malishoni, minadani au sehemu nyingine yoyote;

(e) kuipatia mifugo yake malisho, maji ya kutosha na kuzingatia kanuni za usafirishaji, uuzaji na uchinjaji wa mifugo;

(f) kutoa taarifa yoyote juu ya kutokea kwa magonjwa ya mifugo akiyaona au kuhisi au kuyatambua;

(g) kuogesha mifugo yake kwenye majosho ya pamoja au ya binafsi kulingana na maelekezo ya Afisa Mifugo.

Taratibu wa kuogesha Mifugo

6.—(1) Mifugo itaogeshwa kila baada ya siku kumi na nne (14) na kabla ya kuingia au kutoka nje ya eneo la Mamlaka ya Halmashauri.

(2) Halmashauri itaunda vikundi mbalimbali vitakavyosimamia uendeshaji wa majosho na taratibu za uogeshaji wa mifugo katika maeneo yao ndani ya Halmashauri.

Ushuru wa josho

(3) Mifugo itakayoogeshwa katika majosho ya Halmashauri au Halmashauri za kijiji itatozwa ushuru kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma.

Kibali kusafirisha mifugo

7.—(1) Mtu yeyote anayetaka kusafirisha mifugo kutoka eneo la Manispaa atalazimika kuwa na kibali kitakachotolewa na Halmashauri ili kusafirisha mifugo hiyo.

(2) Kibali cha kusafirisha mifugo nje na ndani ya Manispaa kitatolewa na Afisa Mifugo au Kata au Kijiji baada ya kujiridhisha kuwa mifugo hiyo imeogeshwa na kupatiwa chanjo kabla ya kusafirishwa.

Mifugo inayozurura hovyo

8.—(1) Mifugo yoyote ile itakayokutwa inazurura au inachungwa katika eneo lisiloruhusiwa itakamatwa na kuhifadhiwa na Halmashauri.

(2) Mwenye mifugo atatakiwa kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000)/= kwa kosa la kuchunga mifugo katika eneo lisiloruhusiwa au kuachia mifugo yake kuzurura hovyo na shilingi elfu kumi (10,000/=) kwa kila mfugo, kwa kila siku itakayokuwa chini ya uangalizi wa Halmashauri pamoja na kwa kuachia mifugo yake kuzurura.

(3) Mfugaji atatakiwa kulipa elfu kumi kila siku kwa kila mfugo kwa muda ambao mifugo yake itakuwa inashikiliwa na Halmashauri.

Mafuriko

9. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuingiza mifugo kwenye shamba lenye mazao, kiwanja cha Ndege au eneo lolote lenye marufuku ambalo halikutengwa na Halmashauri katika mpango wa matumizi ya ardhi kama eneo la malisho ya mifugo.

Makosa

10. Mfugaji yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo:-

(a) atashindwa au kukataa kuogesha au kuchanja mifugo yake ili kuzuia magonjwa au;

(b) atazembea au kushindwa kutoa taarifa juu ya ugonjwa wa mifugo au;

(c) atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Afisa Ugani kutekeleza majukumu yake.

Adhabu

11. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000) au kifungo kisichozidi miezi mitatu (3) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa chini ya Sheria Ndogo hizi iwapo mkosaji atakiri kwa maandishi kuwa ametenda kosa hilo na kukubali kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=).

JEDWALI

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

(Chini ya kifungu cha 10)

Mimi ..... nakiri mbele ya .....ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, kwamba mnamo tarehe..... ya mwezi..... Mwaka..... nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha .....cha Sheria Ndogo za Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma (Uthibiti wa Ufugaji Holela) za mwaka 2014.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha Ada/Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYOTOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe ..... ya mwezi .....Mwaka .....
Jina ..... Saini .....

Mbele ya:

Jina:.....
Cheo:.....
Saini:.....

Nembo na muhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 30 mwezi Juni 2011 na kushuhudiwa na:-

ROBERT MATONDO KITIMBO
kurugenzi wa Manispaa ya Dodoma

L.S

EMMANUEL S. MWILIKO
Mstahiki Meya wa Manispaa ya Dodoma

NAKUBALI

DODOMA
03 Aprili, 2014

MIZENGO P. PINDA (MB),
Waziri Mkuu